



JESHI LA POLISI KUIMARISHA HALI YA USALAMA KATIKA MAENEKO YA MRADI WA SGR



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (wa nne kushoto) akimuelezea Mkuu wa Jeshi la Polisi Kamanda Simon Sirro (wa pili kulia) kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Dar es Salaam - Kilosa alipotembelea mradi wa SGR eneo la Vingunguti Dar es Salaam hivi karibuni 2019. Picha zaidi Ukurasa 2.

UFUFUAJI WA RELI YA TANGA - MOSHI - ARUSHA WAPAMBA MOTO



Kazi ya ujenzi wa daraja katika reli ya Tanga - Moshi - Arusha ikiendelea eneo la Hedaru mkoani Kilimanjaro hivi karibuni Machi 2019. Picha zaidi Ukurasa 2



JESHI LA POLISI KUIMARISHA HALI YA USALAMA KATIKA MAENEKO YA MRADI WA SGR



Mkuu wa Jeshi la Polisi Kamanda Simon Sirro akipata maelezo kutoka kwa meneja mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR Dar es Salaam – Morogoro Mhandisi Machibya Masanja kuhusu maendeleo ya ujenzi wa Stesheni kubwa ya treni za kisasa eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam alipofanya ziara kuona hali ya usalama wa mali na wafanyakazi katika mradi wa SGR, hivi karibuni 2019.

UFUFUAJI WA RELI YA TANGA - MOSHI - ARUSHA WAPAMBA MOTO



Shehena ya Makalavati ikiwa tayari katika stesheni ya Mombo kwa ajili ya kupelekwa eneo la ujenzi kukamilisha ukarabati wa reli ya Tanga – Moshi – Arusha.



Kazi ya usukaji madaraja kwa ajili ya ukarabati wa reli ya Tanga – Moshi – Arusha ikiendelea eneo la Hedaru mkoani Kilimanjaro hivi karibuni Machi 2019.



TRC YAENDELEA NA ZOEZI LA ULIPAJI FIDIA ILI KUPISHA UJENZI WA RELI YA KISASA



Mmoja wa wakazi ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR katika eneo la Pugu Stesheni Bwana Omari Said akiweka saini katika kitabu cha malipo ya fidia kabla ya kupokea hundi hivi karibuni Machi 2019.

Shirika la Reli Tanzania laendelea kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam ambao maeneo yao yamepitiwa na Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam – Morogoro katika mitaa ya Guluka Kwalala, Sabasaba, Miembe Madafu na Pugu stesheni.

Shirika linawasisitiza wananchi kuendelea kuwa wavumilivu na kutoa ushirikiano kwa maafisa wa TRC wakati wa zoezi la ulipaji fidia ili kuhakikisha kila mwananchi anayestahili fidia analipwa ili kukabidhi eneo kwa mkandarasi aweze kumaliza Mradi ndani ya muda uliopangwa.



Maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania – TRC pamoja na Afisa Mtendaji wa Mtaa wa Guluka Kwalala wakiendelea na zoezi la ulipaji fidia ya ardhi kwa wakazi wa Mtaa wa Guluka Kwalala katika Kata ya Gongo la Mboto hivi karibuni 2019.



NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA SGR



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mradi wa SGR Dar - Moro Mhandisi Machibya Masanja kuhusu Ujenzi wa Stesheni ya Reli ya Kisasa unaoendelea eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam alipofanya ziara kuona Maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro hivi karibuni 2019.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (wa pili kulia) akiangalia reli ya kisasa - SGR iliyotandikwa eneo la Vingunguti jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2019.



KAMATI YA KUONDOA VIKWAZO KATIKA MRADI WA SGR YAFURAHISHWA NA KASI YA MRADI



Mhandisi Miradi upande wa uondoshaji vikwazo Bwana Alex Bunzu akiwaeleza wajumbe wa kamati ya kuondosha vikwazo katika mradi wa SGR kuhusu daraja la treni ya kisasa linalojengwa kuanzia Stesheni ya Dar es Salaam hadi Ilala walipofanya ziara kuona maendeleo ya mradi hivi karibuni 2019.

Wajumbe wa Kamati ya kuondoa vikwazo katika Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR watembelea kambi za mradi wa SGR za Ilala na Soga kuona maendeleo ya mradi baada ya utekelezaji wa kazi ya kuondoa vikwazo ikiwemo miundombinu ya umeme, mawasiliano, gesi na maji katika maeneo ya mradi, hivi karibuni 2019.

Kamati inaundwa na wahandisi kutoka Shirika la Umeme Tanzania – TANESCO, Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka, Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL, Kampuni za Gesi za SONGAS, PAN AFRICA, RAHA LIQUID na kampuni za simu za TIGO, AIRTEL, ZANTEL na HALOTEL.

